



**UN-HABITAT**

**UJUMBE WA KATIBU MKUU WA UMOJA WA MATAIFA  
SIKU YA MAKAZI DUNIANI (SMD)  
4 OKTOBA 2004**

Mada ya Siku ya Makazi Dunia (SMD) mwaka huu ni “Miji-kama Msukumo wa Maendeleo Vijijini”. Mada hii ilichanguliwa ili kuwakumbusha viongozi katika ngazi zote kuacha dhana kwamba “Miji” na “Vijiji” ni vitu viwili tofauti bali wavione kama vitu vinavyotegemeana kiuchumi na kijamii.

Miji ina mahusiano tegemezi na vijiji kwa njia nyingi tu. Wageni waishio na kufanya kazi mijini hutuma sehemu ya mapato yao vijijini. Na miji huchukua ziada ya wakazi kutoka vijijini, na huwa ni soko la mazao mengi na bidhaa nyinginezo toka huko. Miji hutoa huduma na mahitaji muhimu—kama vyuo vikuu na hospitali, vitu ambavyo mara nyingi havipo katika maeneo ya vijijini. Miji pia ni kiini cha uwekezaji wa kimataifa, kitu ambacho husababisha kuhitajika kwa bidhaa, ajira na vitu vingine muhimu toka vijijini ili kuchangia katika uzalishaji mali.

Katika miaka 25 ijayo, karibu ukuaji wa wakazi wote duniani utajitokeza mijini, na hasa katika miji ya nchi zinazoendelea. Miji inayokua sana itakuwa ni ile ya kati na hasa iliyo karibu na maeneo ya vijiji. Ukuaji huu unaweza kuboresha maisha vijijini na kupunguza matatizo yanayohusishwa na miji mikubwa. Ili kufanya hivyo, tutahitaji utawala bora wa miji, uwekezaji katika mawasiliano, njia nzuri za usafirishaji, na miundo-mbinu nyingine, na jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa watu wote wanafikiwa na huduma muhimu na zinazotosheleza.

Wakati kuna tofauti za wazi katika maendeleo ya miji na vijiji, tofauti hizi zinahitaji kutafutiwa mikakati muafaka kukabiliana nazo ili hatimaye maendeleo endelevu yasiwekwe katika eneo moja au jingine kati ya haya. Wakati tukisheherekea Siku ya Makazi Duniani (SMD), tunalazimika kutambua kuwa miji ina mchango muhimu katika maendeleo vijijini, kwa hiyo basi ni bora sasa tuchukulie maendeleo katika mtizamo wa pamoja na unaonyesha uelewa huo.